**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

# TAARIFA YA UCHUNGUZI YA KAMATI YA MAADILI NA KINGA ZA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MALALAMIKO YA DKT. HASSAN RASHID ALI DHIDI YA MHE ALI SULEIMAN AMEIR

**SEPTEMBA, 2021**

## 1. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, Awali ya yote sinabudi kumshukuru Mwenyezi Mungu Muumba wa viumbe vyote kuweza kukutana tena siku ya leo ndani ya Baraza hili tukufu tukiwa katika hali ya uzima na afya njema huku tukiendelea kujadili mambo muhimu kwa mustakbali wa Taifa letu na wananchi kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, napenda kukushkuru wewe binafsi Mheshimiwa Spika, kwa kutuamini kuifanya kazi hii na kunipa nafasi hii kuwasilisha taarifa hii kwa niaba ya Kamati ya Maadili na Kinga za Wajumbe. Napenda pia kukupongeza wewe pamoja na wasaidizi wako Naibu Spika na Wenyeviti wa Baraza kwa mnavyosimamia kwa umahiri na uadilifu wa hali ya juu ndani ya Chombo hiki cha Uwakilishi wa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 109 fasili ya (15) na Kanuni ya 114 fasili ya (1) na (5) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020, naomba kuwasilisha mbele ya Baraza lako Tukufu Taarifa ya Uchunguzi ya Kamati ya Maadili na Kinga za Wajumbe juu ya Malalamiko ya Dokta Hassan Rashid Ali dhidi ya Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir kuhusu madai ya matamshi yasiofaa ya kadhia ya Mradi wa (ZISP) wakati akichangia Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Mnamo tarehe 17 Juni, 2021 kwa Mamlaka uliyopewa chini ya Kanuni ya 148 fasili ya (2) Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020, uliwasilisha Barazani taarifa ya Mamalamiko ya Dokta Hassan Rashid Ali dhidi ya Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir kuhusu madai ya matamshi yanayodaiwa kuwa yasiyofaa aliyoyatoa tarehe 22 Mei, 2021 ndani ya Ukumbi wa Baraza la Wawakilishi.

**Mheshimiwa Spika,** katika Jadweli la kwanza la Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020 imeeleza Majukumu ya Kamati hii kama ifuatavyo, Naomba kunukuu:

(i) kuchunguza na kuyatolea maamuzi masuala yote yanayohusu kinga, fursa, mamlaka na madaraka ya wajumbe na pia mamlaka na madaraka ya Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Baraza ambayo yamepelekwa mbele ya kamati na Spika au na Mjumbe yeyote wa Baraza.

(ii) mara baada ya kushauriwa na Kamati ya Maadili kwa mujibu wa aya ya (b) ya kanuni hii, Spika atalazimika kukubaliana na ushauri

huo au vyenginevyo kuuwasilisha mbele ya Baraza kwa ajili ya uamuzi.

(iii) kuchunguza na kumshauri Spika juu ya lalamiko lolote kuhusu uamuzi wa Spika, Naibu Spika, au Mwenyekiti wa Baraza ambalo limepelekwa mbele ya kamati hiyo na Mjumbe yeyote.

(iv) mara baada ya kupokea shauri lolote kwa mujibu wa kanuni hii, kamati ya maadili itakutana haraka iwezekanavyo kufikiria na kuchunguza jambo hilo. mwisho wa kunukuu

**Mheshimiwa Spika,** Kufuatia majukumu niliyoyaeleza Kamati yangu ilipokea barua ya tarehe 18/08/2021 yenye kumbukumbu BLW/K/10/13/67 yenye maelezo ya hadidu rejea kwa ajili ya kuyafanyia kazi malalamiko yaliyowasilishwa kama ifuatavyo:

(i) kuchunguza iwapo maneno ya Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir aliyoyasema wakati akichambua bajet ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na katika Kamati ya matumizi mnamo tarehe 22 Mei, 2021, ni maneno yasiyofaa na yanakiuka Kanuni ya 60 ya Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020.

(ii) kuchunguza iwapo Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir amekiuka kanuni za Maadili ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kama zilivyoelezwa na Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020. na sheria nyengine zinzohusika kutokana na maneno yake dhidi ya Dokta Hassan Rashid Ali wakati akichangia Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na katika Kamati ya Matumizi ya Baraza la Wawakilishi mnamo tarehe 22 Mei, 2021.

(iii) kuchunguza iwapo Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir amemdhalilisha mlalamikaji Dokta Hassan Rashid Ali kwa maneno aliyoyasema wakati anachangia bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Kamati ya Matumizi, tarehe 22 Mei, 2021.

## 2. CHIMBUKO LA MALALAMIKO

**Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 22 Mei, 2021 katika Baraza la Kumi, Mkutano wa Tatu, kikao cha kumi na tatu wakati wa kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir kupitia kanuni ya 99 (4) Alizuwia vifungu na kuomba kupatiwa ufafanuzi wa kina kuhusiana na mradi wa ZISP unaotekelezwa na SUZA na kumtaja Mshauri Elekezi Dokta Hassan Rashid Ali wakati akinukuu barua iliyoandikwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kumpelekea Makamo Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa iliyoelezea

maagizo ya Baraza la Mapinduzi, ambayo ilimtaka arejeshe fedha alizopewa kinyume na utaratibu wakati wa utekelezaji wa Mradi.

**Mheshimiwa Spika,** siku iliyofuata tarehe 23 Mei, 2021, Mlalamikaji Dokta Hassan Rashidi Ali aliandika barua iliyodai kuibuliwa kwa suala la mradi wenye deni ambalo Serikali imeagiza lilipwe lakini bado halijalipwa. Mlalamikaji alidai kuchafuliwa kwa makusudi na Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir kwa jamii kupitia vyombo vya habari kinyume na sheria na taratibu na kutumia vibaya kinga yake kisheria ndani ya Baraza. Kutoheshimu haki za wengine kwa kutajwa majina yao hadharani bila ya kuwa na ushahidi wa tuhuma zilizotajwa juu ya hukumu iliyotolewa na Serikali kuhusu Kadhia hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Dokta Hassan Rashid Ali katika malalamiko yake alieleza ni muhimu Wawakilishi wasibebe mambo wanayolishwa na kuja kuyatetea kwa jazba bila ya kufanya uchunguzi wa kina. Aidha, alisema Baraza linataka kutumiwa vibaya au kupotoshwa na kuchukua nafasi ya Mahakama ambayo hata kesi haijapelekwa.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya Maelezo hayo na kupatiwa hadidu rejea zilizoambatana na vielezo vya kufanyia kazi, Kamati ilikutana rasmi kuanzia tarehe 30 Agosti, 2021 hadi tarehe 14 Septemba, 2021, kwa ajili ya kufanyia kazi hadidu rejea zilizowasilishwa kuhusiana na malalamiko hayo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Sheria ya Kinga na fursa za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2021, kifungu cha 14 kinatoa fursa ya kumwita mtu yeyote kuhudhuria mbele ya Kamati kutoa ushahidi au nyaraka anayoimiliki.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliwaita Mashahidi wawili wanaohusika na kadhia hiyo ili wafike mbele ya Kamati kwa mahojiano wakiwa na vielelezo na uthibitisho wa barua au nyaraka zinazohusiana na mradi mzima wa ZISP.

**Mheshimiwa Spika,** siku ya tarehe 3 Septemba, 2021 wakati Kamati ikiwasikiliza mashahidi hao, Kamati pia iliwaita mashahidi wengine tisa kwa siku tofauti kama ifuatavyo:

(i) Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali;
(ii) Bi. Khadija Bakari, Katibu Mkuu Mstaafu wa Wizara ya Elimu;
(iii) Dokta Idrisa Muslih Hija, Katibu Mkuu Mstaafu wa Wizara ya Elimu;
(iv) Profesa Idris Ahmada Rai, Makamo Mkuu Mstaafu wa SUZA;
(v) Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali;

(vi) Dokta Zakia M. Abubakar, Makamo Mkuu wa Chuo cha SUZA;
(vii) Dokta Ali Makame Ussi, kutoka chuo cha SUZA;
(viii) Dokta Haroun Ayoub Maalim, kutoka Chuo cha SUZA;

**Mheshimiwa Spika,** mashahidi hao pia walipatiwa Barua za wito zilizowataka kufika mbele ya Kamati kwa mahojiano kuhusiana na kupishana kwa baadhi ya taarifa zilizojitokeza wakati mashahidi wa awali wakihojiwa.

## 3. UCHAMBUZI WA HADIDU REJEA ZILIZOFANYIWA KAZI NA KAMATI

### (a) HADIDU REJEA YA KWANZA

***Mheshimiwa*** **Spika,** hadidu rejea ya kwanza iliyopewa Kamati kuifanyia kazi ni *kuchunguza iwapo maneno ya Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir aliyoyasema wakati akichangia Bajet ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na katika Kamati ya matumizi mnamo tarehe 22 Mei, 2021, ni maneno yasiyofaa na yanakiuka Kanuni ya 60 ya Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020.*

***Mheshimiwa*** **Spika,** Kamati ya Maadili katika kuifanyia kazi hadidu hii imeanza kwa kuyachunguza maneno ya Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir aliyoyasema siku ya tarehe 22 Mei, 2021 kwa kuyanukuu katika hansad kama ifuatavyo:

*"Mhe. Mwenyekiti, nchi hii ina mihimili mitatu; Executive, Judiciary and Parliament. Executive imeshatoa maamuzi kuwaambia watendaji tunataka fedha zetu zirudishwe ambazo zimetumika ipasavyo. Kwa agizo lililotolewa na Baraza la Mapinduzi kupelekwa kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wawatake SUZA pesa za watu zilizotumika za mradi zirudi dola 445,000. Hili linatokana na ripoti tatu, Ripoti ya Ukaguzi wa Mradi, Ripoti ya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali CAG na linatokana na Ripoti ya Maamuzi ya Bodi yenyewe ya SUZA. Yapo yaliyotekelezwa mawili hayajatekelezwa. Naomba anijibu haya.*

*Mhe. Mwenyekiti, SUZA irejeshewe fedha zake zote ilizopaswa kupata kutokana na mradi huu kutoka kwa Dokta Hassan Rashid Ali aliyepewa fedha na SUZA kinyume na taratibu kulingana na Sera na Taratibu za Chuo, kuhusu wataalamu wa chuo wanapopewa kazi kama hiyo kupitia chuo na kutumia rasilimali za chuo. Hiyo moja haijatekelezwa mpaka leo.*

*Nne, fedha zilizotumika kinyume na utaratibu wahusika watakiwe kuzirudisha na kama hawakufanya hivyo, wakatwe moja kwa moja kutoka katika mishahara yao.* ***Sio maneno yangu,*** *hayo ni maneno ya Executive, ni maneno ya Katibu Mkuu wa Wizara anaiambia SUZA,*

*ameapa huyo viapo vitatu. Ameapa wakati anakabidhiwa certificate ya ushindi ya Chama cha Mapinduzi ataweza kutekeleza yote, ameapa ndani ya Baraza hili atasikiliza na maamuzi yote yatakayotolewa mbele ya Mhe. Rais, atachukua maagizo ambayo yataamuliwa na Mhe. Rais na chombo chake. Ninachotaka aniambie dogo tu, dola zetu 445,959 sawa na shilingi 1,052,463,240 zitarudishwa lini tukazitumie katika Uimarishaji wa Elimu ya Sekondari.". Mwisho wa kunukuu.*

***Mheshimiwa* Spika,** Kamati imeyapitia maneno hayo na katika kuyatafakari tumeona kwamba Mjumbe anayo haki ya kuchangia kwa mujibu wa kifungu cha 3 cha Sheria Nam.4 ya mwaka 2007 ambacho kimetoa uhuru wa Mjumbe kujadili na kuchangia, na uhuru huo hawezi kuhojiwa kwenye Mahkama ya Sheria au pahala pengine popote nje ya Baraza, ambayo inaeleza:

*"Kwa mujibu wa masharti ya Kanuni za Kudumu za Baraza zinazoendesha shughuli za Baraza, kutakuwa na uhuru wa kujieleza na kujadiliana kwenye Baraza na uhuru huo na majadiliano hayo hautahojiwa katika Mahkama yoyote ya Sheria au pahala pengine popote nje ya Baraza".*

Hivyo, baada ya kuyasoma na kuyasikiliza maneno ya Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir, Kamati haikuwa na shaka kuwa alitumia uhuru wake wa kisheria iliyotajwa hapo juu kuyawasilisha.

**Mheshimiwa Spika,** Mbali na Hansad, kamati imetizama maelezo hayo ya mchango wa Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir kupitia rekodi ya video ya kikao cha tarehe 22/5/2021 na kuchunguza namna yaliyoelezwa na Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir na kuyafahamu zaidi.

Hayo yote yamechunguzwa ili kubainisha hadidu rejea hii kama itathibitishwa uvunjwaji wa Kanuni ya 60 au la na katika kufanya hivyo kamati imetaka kufahamu iwapo maneno haya yamekiuka kanuni ya 60(3) ambayo inasema:

> "*Mjumbe yeyote anapokuwa akizungumza Barazani atawajibika kuwa na sababu za msingi kwamba maelekezo anayoyatoa ni sahihi na sio mambo ya kubuni au ya kubahatisha tu, na Spika au Mjumbe mwengine yeyote anaweza kumtaka Mjumbe huyo atoe uthibitisho wa usemi wake unaohusika."*

Kanuni hii kwa ujumla inazungumzia mambo yanayofaa na yasiyofaa kuzungumzwa ndani ya Baraza la Wawakilishi wakati Mjumbe anaposema.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeichambua Kanuni ya 60(3) ili kuthibitisha kama imevunjwa kutokana na maneno ya Mheshimiwa Ali Suleima Ameir na Kamati ilifanya uchambuzi huo kwa kutizama maeneo makuu matatu yafuatayo:

- Je, maelezo ya Mheshimiwa ni sahihi;
- Je, maelezo hayo siyo ya kubuni na kubahatisha; na
- Je, ameyathibisha.

**Mheshimiwa Spika,** Baraza likumbuke kuwa Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir alitoa maelezo yake sehemu mbili, kwanza wakati akichangia hoja ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na baadae wakati akichangia Kamati ya Matumizi aliposimama kutaka ufafanuzi wa hoja alizotangulia kuchangia ambazo hazikupata majibu ya kutosha. Jina la Dokta Hassan Rashid Ali lilitajwa kwenye sehemu ya pili ya mchango wa Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir ambao ulikuwa kwenye kamati ya matumizi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipomhoji mlalamikaji alieleza kuwa maelezo ya Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir hayakuwa sahihi kwa vile yeye hadaiwi na SUZA wala hakuiba fedha hizo, kwa hivyo hakuna haja ya yeye kurejesha fedha kama alivyodai Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir.

**Mheshimiwa Spika,** Kuhusu hoja hiyo Kamati pia ilimhoji shahidi mlalamikiwa Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir ambaye alieleza kuwa maelezo aliyoyasema ni sahihi na aliyanukuu kutoka kwenye barua aliyopelekewa Makamo Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA) kutoka kwa Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ambayo Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir alisema kuwa ana kila sababu ya kuyaamini maelezo hayo kuwa ni sahihi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilichambua zaidi na kutizama kama kuna pahala popote kwenye maelezo ya Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir amemtaja Dokta Hassan Rashid Ali kama "ameiba" au "anadaiwa" kama alivyofafanua Dokta Hassan Rashid Ali wakati akihojiwa na Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwa mujibu wa kumbukumbu za Kikao ya "hansard" ya maandishi na rekodi ya Video ambazo mashahidi wote hao walipatiwa hakuna pahala ambapo Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir amemtaja au kuashiria kama Dokta Hassan Rashid Ali ameiba au anadaiwa fedha hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeona maneno aliyotumia Mheshimiwa ni *"……..aliyepewa fedha….."* ambayo hayaleti tafsiri ya kuwa Dokta Hassan Rashid Ali ameiba, anadaiwa au amechukuwa fedha hizo.

Maneno hayo aliyoyanukuu kutoka katika barua hiyo awali kabla ya kuyasema aliwasilisha vielelezo vyake kwa Naibu Spika siku ya tarehe 22/05/2021, na kwenye Kamati wakati akihojiwa. Hivyo, kwa maana hiyo Kamati iliridhika kuwa maelezo yale yalikuwa sahihi na yalithibitika kwa vielelezo hivyo vilivyowasilishwa kwenye Baraza wakati Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir akichangia na pia kuwasilisha vielelezo vyake wakati kamati ya Maadili ikimuhoji.

**Mheshimiwa Spika,** Katika sehemu ya pili ya uchambuzi wa Kanuni ya 60(3) Kamati ilijielekeza pia kuchambua kama maelezo ya Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir yalikuwa ya kubuni au yakubahatisha, katika kuchunguza suala hilo, Kamati ilimsikiliza Shahidi wa kwanza Mlalamikaji Dokta Hassan Rashid Ali ambae alisema "Tuhuma za Mheshimiwa hazina ushahidi" rejea barua ya mlalamikaji ya tarehe 23/5/2021 kama *(kielelezo namba 1.)* Maana yake ni sawa na Shahidi huyo kudai kuwa maelezo ya Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir yalikuwa ya kubuni na kubahatisha kinyume na Kanuni ya 60 (3).

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuchambua zaidi hoja hii, kamati imechunguza sehemu ya hoja ya Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir wakati akikazia maelezo yake katika Kamati ya matumizi alisema *"………sio maneno yangu, si maneno yangu……."* kauli hii ilionesha Mheshimiwa akisema huku ameshika karatasi ambayo alikuwa akinukuu maneno hayo ambayo kamati ilipotaka kielelezo cha karatasi ilipatiwa. Hivyo, kamati imejiridhisha kuwa maneno hayo hayakuwa mambo ya kubuni wala kubahatisha kwavile yalinukuliwa katika chanzo sahihi na wala aliyeyaandika Dokta Idrissa Muslih Hija hakuyakanusha wakati alipohojiwa na Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Sambamba na hilo, kamati ilipata fursa ya kuichunguza Ripoti ya Ukaguzi Maalum wa Mradi wa Uimarishaji wa Mazingira ya Kujifunzia Wanafunzi Zanzibar (ZISP) ambapo Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir aliegemea maelezo yake wakati akiwasilisha hoja yake ambayo ni kweli kuwa ilikuwa na mapendekezo ambayo Mheshimiwa aliyaeleza Barazani. *(Kielelezo nam. 2)*

Aidha, kamati imethibitisha kuwa Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir hakukiuka Kanuni ya 60 wakati akitoa maelezo yake kwa vile Kamati ilithibitisha kwa maelezo na vielelezo kuwa maneno aliyoyasema yalikuwa sahihi, hakuyabuni wala hakuyabahatisha.

**(b) HADIDU REJEA YA PILI**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imetakiwa *kuchunguza iwapo Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir amekiuka kanuni za Maadili ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kama zilivyoelezwa na Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020 na sheria nyengine zinzohusika kutokana na maneno yake dhidi ya Dokta Hassan Rashid Ali wakati akichangia Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na katika Kamati ya Matumizi ya Baraza la Wawakilishi mnamo tarehe 22 Mei, 2021.*

**Mheshimiwa Spika,** Katika kufanyia kazi hadidu rejea hiyo, kamati ilichunguza maneno ya Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir kama yamekiuka Kanuni za Maadili na Sheria nyengine. Kanuni za Maadili zimetajwa katika Kanuni ya 67(2) ya kanuni za kudumu inasema:

*"Mjumbe atawajibika pia kufuata kwa ukamilifu Kanuni za Maadili zilizopo kwenye Jadweli la Pili la Kanuni hizi (Kanuni za Kudumu za Baraza)".*

**Mheshimiwa Spika,** Sheria nyengine zilizokusudiwa na kamati kwa mnasaba wa hadidu rejea hiyo imetambua kuwa ni kifungu cha13 cha Sheria namba 4/2007 ya Kinga na Fursa za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kinacholipa uwezo Baraza kuweka Kanuni za Maadili na kifungu cha 18(1) (ix) cha Sheria namba 4 ya mwaka 2015, Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, ambacho kinakataza Kiongozi wa Umma (wakiwemo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi) kutumia lugha ya kushutumu na matusi.

**Mheshimiwa Spika,** lengo la kanuni za maadili kuwasaidia wajumbe katika utekelezaji wa majukumu yao kwenye Baraza, majimbo na katika jamii kwa ujumla. Kamati imepitia kwa makini vipengele vyote 12 vya kanuni za maadili kama ilivyo kwenye Jadweli la pili la Kanuni za kudumu za Baraza (*kielelezo namba 3).*

**Mheshimiwa Spika,** katika eneo hili kipengele cha 11 kinahusika cha kanuni za maadili kinachosema:

*"Wajumbe ni wajibu wao kukumbuka kwamba taarifa wanazozipokea katika utekelezaji wa makujumu yao kwa mujibu wa nafasi zao, wakiaminiwa wakiwa Wawakilishi wa Wananchi wanapaswa kuzitumia taarifa hizo kwa lengo hilo tu la kutekeleza majukumu yao na kamwe taarifa hizo zisitumike kwa ajili ya kujipatia umaarufu wala kujipatia maslahi ya kifedha".*

**Mheshimiwa Spika,** katika mahojiano ya shahidi Mlalamikaji na vielelezo vyake hakusema kuwa Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir ametumia taarifa alizopata kujipatia umaarufu wala maslahi binafsi ya kifedha. Kamati ilichobaini ni kuwa Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir amehoji uwepo wa fedha ambazo zilitakiwa kurejeshwa SUZA na kutokana na taarifa alizowasilisha, fedha hizo hazijarudishwa pamoja na kuwepo maagizo ya maandishi, ambayo ameyanukuu, ya kutaka fedha hizo zirejeshwe. Hivyo, maelezo hayo ni dhahiri kuwa hayajakiuka Kanuni za Maadili za Baraza kama zilizotajwa kwenye Jadweli la Pili la Kanuni.

**Mheshimiwa Spika,** kwenye Sheria ya Maadili kifungu cha 18(1) (ix) kimekataza kiongozi kutumia lugha ya kushutumu na matusi/ukali. Suala hili limetizamwa pamoja na kanuni ya 60(8) ambayo itaelezwa kwa kina kwenye hadidu rejea ya tatu inayofuata ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni za maadili kipengele cha 11 kimetaja tu namna ya Mjumbe kutumia taarifa lakini namna ya Mjumbe kupata taarifa haikueleza, isipokuwa Sheria namba 4 ya 2007 imeweka utaratibu huo katika kifungu cha 9 cha Sheria hiyo. Hata hivyo, Kamati ya Maadili imebaini jambo moja ambalo kwa fursa hii tunaelezea ili kuwafahamisha wajumbe wengine kuchukua utaratibu wa kisheria wa Mjumbe kupata taarifa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipomhoji shahidi mlalamikiwa Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir kuhusu wapi alipata taarifa na kama amefuata utaratibu kuzipata, alieleza kuwa ametumia njia zake mwenyewe kupata taarifa hizo.

Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir alifahamisha Kamati kuwa anayo haki kwa mujibu wa kifungu cha 23(2) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ambacho kimempa wajibu kama Mwakilishi kushiriki katika ulinzi wa mali za Serikali na alitimiza wajibu huo kwa kuona kuwa fedha za wananchi zipo hatarini kupotea hivyo alikuwa na wajibu wa kupaza sauti na kulinda. Kifungu hicho cha Katiba kinaeleza kuwa:

*"Kila mtu ana wajibu wa kulinda maliasili ya Zanzibar, mali ya nchi na mali yote inayomilikiwa kwa pamoja na wananchi, na pia kuiheshimu mali ya mtu mwengine".*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilichambua maelezo hayo wala haina tatizo na mwananchi yeyote kutimiza wajibu wa kikatiba kulinda mali za umma, wala Kamati haikuwa na wasiwasi. Isipokuwa dhamira na nia yake safi ya Mheshimiwa Ali Suleiman kuwasilisha hoja zake kwa msingi alioutumia. Kamati iliona tatizo ni kuwa Mheshimiwa Ali

Suleiman Ameir hakufata utaratibu sahihi wa kupata taarifa alizotumia kuwasilisha hoja zake Barazani.

**Mheshimiwa Spika,** ikumbukwe kuwa Mheshimiwa Ali ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa kifungu **cha 65 (a)** cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ambaye ana kinga ya kisheria kwa mujibu wa Sheria namba 4 ya mwaka 2007 na kifungu cha 88 cha Katiba kinampa haki ya kufanya majukumu yake ya uwakilishi.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na hayo utaratibu wa kisheria wa Mjumbe yeyote wa Baraza umewekwa katika kifungu cha 9 cha Sheria namba 4 ya mwaka 2007 ambacho kimetoa haki ya mjumbe kupata taarifa. kifungu hicho kinaeleza kama ifuatavyo:

*"Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii na masharti ya Sheria nyengine zinazohusiana na usalama wa Serikali, Mjumbe atapatiwa taarifa anazozitaka kutoka kwa Ofisa wa Umma".*

**Mheshimiwa Spika,** Mheshimiwa Ali alipotoa maelezo yake hakutaja kuwa alipata taarifa hizo kwa utaratibu wa kifungu hiki ambacho utekelezaji wake unataka Mjumbe amuandikie Katibu wa Baraza la Wawakilishi, ambae atawasiliana na Taasisi husika ili kuomba kupatiwa taarifa hizo. Kwa vile jambo hili halikuwa sehemu ya malalamiko isipokuwa kamati imeliibua kwa nia ya kutoa ushauri tu, Kamati haitapendekeza adhabu yoyote kwakuwa utaratibu wa kisheria ni kuwa mtu hawezi kuadhibiwa kwa kosa ambalo hajashitakiwa hata kama amelifanya.

**Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo, itakuwa busara kutumia taarifa hii na wajibu wa kamati hii kufahamisha kuwa wajumbe wa Baraza wanapotaka kupata taarifa wafuate masharti ya kifungu cha 9 cha Sheria namba 4 ya mwaka 2007 kwa utaratibu ulioelezwa hapo juu, kufanya hivyo kutaepusha wajumbe kupokea taarifa za uwongo au kupotosha au za siri ambazo mtoaji hakupewa idhini azitoe.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa SUZA ambako inaonekana taarifa hizo ndiko zilikotokea, Kamati iliwahoji wahusika na imebainika kuwa na wao hawakufuata utaratibu wa kutoa taarifa hizo za Ofisi. Kwa mujibu wa kifungu cha 53 cha Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2014 kimekataza na kupiga marufuku kwa Mtumishi wa Umma kutoa taarifa za Ofisi bila kupata idhini ya Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi. Kifungu hicho kinaeleza:

*"Ni marufuku na hairuhusiwi kwa mtumishi yeyote wa umma kutoa kumbukumbu za taasisi zilizomo ndani ya majalada bila ya kupata kibali cha Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi".*

## (c) HADIDU REJEA YA TATU

**Mheshimiwa Spika,** Katika hadidu rejea ya tatu Kamati imetakiwa *kuchunguza iwapo Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir amemdhalilisha mlalamikaji Dokta Hassan Rashid Ali kwa maneno aliyoyasema wakati anachangia bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Kamati ya Matumizi, tarehe 22 Mei, 2021.*

Kamati katika kuifanyia kazi hadidu hii ilitaka kujua iwapo mlalamikaji amedhalilishwa, katika kuchunguza huko imeiangalia kwa undani hadidu rejea ya kwanza na pili zilivyothibitika;

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi zimeweka utaratibu na kiwango cha lugha inayotakiwa kutumiwa na Wajumbe wanaposema Barazani au kwenye Kamati. Viwango hivyo vya matumizi ya lugha vimewekwa katika Kanuni ya 60 (8) ambayo inasema:

"Nimarufuku kwa Mjumbe yeyote:

(a) kutumia lugha au ishara ya matusi, kejeli, kashfa au lugha isiyokuwa ya staha itakayolishushia hadhi na heshima Baraza, Serikali pamoja na yeye mwenyewe.

(c) kumzungumza mjumbe au mtu mwengine kwa nia mbaya au kumshambulia binafsi, isipokuwa kwa kutoa hoja halisi inayohusu mwenendo mahsusi wa mjumbe huyo".

**Mheshimiwa Spika,** Malalamiko ya Dokta Hassan Rashid Ali kwa mujibu wa barua aliyomuandikia Mheshimiwa Spika tarehe 23/05/2021 ni kuwa amechafuliwa kwa makusudi na Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir. Kamati ilipomuhoji na kumtaka Dokta Hassan Rashid Ali, Mlalamikaji afafanue ni kwa namna gani maneno ya Mheshimiwa yamemchafua na kumdhalilisha.

**Mheshimiwa Spika,** Dokta Hassan Rashid Ali alieleza kuwa kile kitendo cha kutajwa jina lake kwenye Baraza, watu wa ndani na nje ya nchi wanaomfahamu na waliofatilia kikao kile walisikia maelezo yale na kuona kuwa yamemchafua. Alieleza kuwa yeye ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu, anaheshimiwa na watu mbalimbali pamoja na wanafunzi wake, kutajwa katika Baraza kuwa anatakiwa arejeshe fedha wakati hajaiba wala hadaiwi kumemdhalilisha mbele ya watu hao na jamii kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Dokta Rashid Hassan Ali aliendelea kueleza kwamba Mheshimiwa hakuwa anafahamu ukweli wote kuhusu jambo

lile kwa maana (mradi wa ZISP) alitakiwa afatilie zaidi kujua baada ya hatua ya kutakiwa walipe kitu gani kimefuata kabla ya kueleza maneno yale na kumtaja jina. Alisema kuwa hakuwa na tatizo endapo jina lake lisingetajwa. Shahidi huyo mlalamikaji alibainisha kuwa haikuwa sahihi kwa Mheshimiwa kusema yeye amepewa fedha kinyume na utaratibu.

**Mheshimiwa Spika,** kwenye madai yake Dokta Hassan Rashid Ali alilalamika kuwa barua aliyoisoma Mheshimiwa Ali ni barua binafsi walizoandikiwa na SUZA walipe ambazo Mheshimiwa alisingizia kuwa ni maamuzi ya Baraza la Mapinduzi, barua hizo za SUZA yeye Dokta Hassan na wenzake walishazikataa kwa maandishi kuwa hawadaiwi, hawatolipa na hawapo tayari kukatwa mishahara yao**.** *(kiambatanisho namba 4).*

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na malalamiko hayo ya Dokta Hassan, Kamati ilimsikiliza mlalamikiwa shahidi wa upande wa pili Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir kuhusu malalamiko hayo. Mheshimiwa Ali Suleima Ameir alieleza kuwa maneno yake hayajamdhalilisha Dokta Hassan, wala yeye hakumtaja jina lake isipokuwa alinukuu barua ambayo jina lake limeandikwa kwenye barua ile.

**Mheshimiwa Spika,** kamati ilipomuhoji kuwa kusikika jina la Dokta Hassan hadharani kama vile alivyomtaja kumesababisha ajione kuwa amedhalilika, Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir alieleza kuwa wakati anachangia jina la Dokta Hassan halikuwa kichwani kwake wala hamjui na wala hakukusudia kulitaja, bali wakati wa kamati ya matumizi alilazimika kufanya nukuu ya barua ili kutilia nguvu hoja yake ambayo haikupatiwa majibu mazuri na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipomuhoji kama maelezo yake hayakulenga kumshutumu Dokta Hassan yalikuwa yakimshutumu nani? Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir aliieleza Kamati kuwa hakuwa anamshutumu yeyote, Siyo SUZA, Serikali, Wizara wala Dokta Hassan lilikuwa suala la ufatiliaji na utekelezaji wa yale maagizo tu.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na maelezo hayo Mheshimiwa Ali Suleiman alieleza kuwa barua ya malalamiko ya Dokta Hassan Rashid Ali ilimdhalilisha kutokana na kuwa barua hii ilitumwa nakala katika sehemu mbalimbali ikiwemo kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambaye pia ni Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa SUZA, Mheshimiwa Makamo wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Katibu

Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

**Mheshimiwa Spika,** Sambamba na lalamiko hilo Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir alilalamika kuhusu utumiaji wa lugha usio sahihi wakati akijibiwa hoja yake na Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, alilalamikia kuwa maneno aliyoyatumia Mheshimiwa Waziri ambayo. Naomba kuyanukuu:

*"Mheshimiwa najua* ***amevimba*** *anataka majibu,* ***ametuna*** *ina maana ana* ***hasira*** *na jambo hili".* Mwisho wa kunukuu

Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir alisema maneno haya yamemdhalilisha na alitaka Waziri amuombe radhi. Hata hivyo Kamati ilipomhoji Mheshimiwa Waziri alisema hakukusudia vibaya kauli hiyo lakini iwapo Mheshimiwa Ali amekwazika kutokana na kauli hiyo. Kwa nafasi hii **Kamati inapendekeza kwa Mheshimiwa Spika amtake Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kumuomba radhi Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir kwa kauli hiyo**.

**Mheshimiwa Spika,** Katika uchambuzi wa kitaratibu na kikanuni wa maelezo hayo yote Kamati iliyapima maelezo ya pande zote mbili kwa kutumia kanuni ya 60(8) (a) na (c) ambazo zinamkataza mjumbe anaposema barazani kutotumia lugha au ishara ya matusi, kejeli, kashfa au lugha isiyo na staha itakayolishushia hadhi Baraza, Serikali pamoja na yeye mwenyewe. Aidha, Kanuni ya 60(8) (c) Mjumbe anakatazwa kumzungumza Mjumbe au mtu mwengine kwa nia mbaya au kumshambulia binafsi.......".

**Mheshimiwa Spika,** katazo hilo limelenga kulinda heshima ya Mjumbe na watu binafsi iwapo Mjumbe hatofanya hayo basi tendo lake haliwezi kuhesabiwa kuwa amemdhalilisha mtu au Mjumbe. Mambo mawili makubwa yanaleta shida katika maneno ya Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir, kwanza, kutaja jina la Dokta Hassan Rashid Ali, pili kusema amepewa fedha kinyume na utaratibu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imepima kama mambo hayo mawili ni kashfa, kejeli au matusi au hayakuwa ya staha au maneno hayo yalimshambulia Dokta Hassan binafsi hali ambayo ingempelekea kudhalilika. Kanuni za Baraza hazikatazi kutaja mtu kwa utaratibu kuwa kama kuna ushahidi wa kile kinachofanya mtu huyo atajwe kama vile kuwepo hoja maalumu ya kuhusu mtu huyo.

**Mheshimiwa Spika,** sehemu ya maneno aliyosema Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir naomba kunukuu *"………SUZA irejeshewe fedha zake zilizopaswa kupata kutokana na mradi huu kutoka kwa Dokta Hassan*

*Rashid Ali aliyepewa fedha kinyume na utaratibu.....”* maneno hayo ukiyasikia huoni shutma kwa uwazi, kwa vile hayasemi kuwa Dokta Hassan ndiye aliyekuwa hakufata utaratibu kwa vile yeye ni mpokeaji tu na hakuiba wala kuzichukuwa bali alipewa. Kwa mantiki hiyo, Dokta Hassan hakushutumiwa kwa kuiba wala kukopa au kuchukua fedha hizo, maelekezo yalitaka fedha irejeshwe kwa kuwa aliyetoa kumpa Dokta Hassan hakufata utaratibu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati wakati inamuhoji Katibu Mkuu mstaafu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali endapo maneno hayo yanamdhalilisha Dokta Hassan alisema kuwa kama fedha zimetolewa kinyume na utaratibu, basi anayehusika ni *“Accounting Officer”* anayeidhinisha siyo Dokta Hassan aliyepokea. Ingawaje Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir ameiambia Kamati kuwa hakumlenga mtu lakini maneno yale kama yanawekwa pahala husika basi mpewaji wa hizo fedha hayamuhusu bali aliyetoa fedha hizo ambaye ni Makamu Mkuu wa Chuo (SUZA).

## 4. UKWELI WA FEDHA KUTOLEWA KINYUME NA UTARATIBU

**Mheshimiwa Spika,** Katika maelezo yake Dokta Hassan ameomba kadhia hii iangaliwe kwa uangalifu kwa maana kuwa yapo mambo mengi ambayo Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir hakuwa na taarifa nayo au hakuyaeleza. Suala la kutolewa fedha kinyume na utaratibu imekuwa ndio eneo lenye kuzusha hali ya malalamiko. Kamati ilitaka kujua ukweli wake hasa ukoje.

Kamati ilipata fursa ya kuupitia Mkataba uliofungwa baina ya SUZA na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali *(Kiambatanisho nam. 5)* ambao ndio msingi mkuu wa kazi ya ushauri elekezi. Katika Mkataba huo kamati ilichunguza utiaji wa saini, utekelezaji wake, udhaifu wake na kasoro zake.

**Mheshimiwa Spika,** Kwenye suala la utiaji saini kamati imebaini Mkataba huo ulitiwa saini na Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wa wakati huo Bi Khadija Bakari Juma kwa upande mmoja na upande wa Chuo Kikuu Mkataba ulisainiwa na Dokta Hassan Rashid Ali kwa niaba ya SUZA. Jambo ambalo Kamati imeona ilikuwa kinyume na Sheria kwa mujibu wa Sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa, kifungu cha 13 (3) cha Sheria Nam. 8 ya mwaka 1999.

**Mheshimiwa Spika,** Chuo Kikuu cha Taifa ni chombo kinachojitegemea kwa mujibu wa kifungu cha 3 kwamba SUZA ina uwezo wa kuingia Mkataba, kushtaki na kushtakiwa, ambapo mtendaji mkuu ndie Makamo Mkuu wa Chuo na ndiye Afisa Muhusika wa kufunga Mkataba huo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mnasaba huo Kamati imeona kwamba Dokta Hassan Rashid Ali hakuwa mtu sahihi wa kusaini mkataba wa kazi hiyo kwa

niaba ya chuo na hakuwa na idhini ya maandishi inayomhalalisha kusaini Mkataba. Uchambuzi huu wa Kamati unaungwa mkono na Ripoti ya Ukaguzi Maalumu wa Mradi wa Uimarishaji wa Mazingira ya kujifunzia wanafunzi Zanzibar ambayo pia imebainisha dosari hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa utekelezaji kamati ilipata maelezo kupitia mashahidi mbalimbali akiwemo Dokta Hassan ambae aliamini ya kwamba kwakuwa yeye ndie aliyeweka saini kwa niaba ya Chuo basi ndie Msimamizi Mkuu wa utekelezaji wa mradi huo.

**Mheshimiwa Spika,** Dokta Hassan alipohojiwa kadhia hii alieleza kuwa hakuna utaratibu uliokiukwa katika Mradi wa ZISP wao waliomba baada ya zabuni kutangazwa kwenye gazeti la Zanzibar Leo *(Kiambatanisho namba 6)* ambao mtu yeyote mwenye sifa angeliweza kuomba. Alisema kuwa walifata taratibu zote za kuomba zabuni mpaka kujaza mkataba.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, Dokta Hassan alieleza kuwa Chuo cha SUZA kina sera yake kuhusu kazi za ushauri elekezi ambayo inaelekeza (*kiambatanisho namba 7)* kuwa mradi utakaotafutwa na Chuo utakuwa kwenye dhamana ya Chuo na ule utakaotafutwa na wafanyakazi na wataalamu wa Chuo utakuwa dhamana yao ambapo Chuo kitapata asilimia 15 ya faida.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wake Katibu Mkuu Mstaafu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Bi Khadija Bakari Juma alieleza alipata barua kutoka kwa Makamo Mkuu wa Chuo wa wakati huo ikiwatambulisha Dokta Hassan Rashid Ali na mwenzake kuwa washauri elekezi wa mradi. (*kiambatanisho barua 8)* Pamoja na maelezo hayo na mawasiliano mbalimbali ya barua ambazo zilitumwa kutoka Wizara ya Elimu kwenda chuo cha Taifa zilionesha wazi kuwa kazi hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya Chuo na si ya mtu binafsi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilipata kumuhoji Dokta Makame Ali Ussi ambaye alieleza mambo mbalimbali kuhusu mradi wa ZISP na alieleza kuwa yeye alikuwa Mjumbe wa Baraza la Chuo akiwakilisha Seneti, jambo hilo lilipokuja kwenye Baraza walimuuliza Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wa wakati huo kuhusu nani walikusudia kuingia naye Mkataba, naye alijibu kuwa Mkataba huo ulikuwa baina ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA).

**Mheshimiwa Spika,** Dokta Ali Makame Ussi aliendelea kuelezea kuwa tatizo kubwa alilobaini katika kadhia hii ni kutofuatwa kwa utaratibu, baadhi ya wahusika ni wazito katika kufuata utaratibu na akitokea mtu kusimamia utaratibu anaonekana mkorofi. Alizidi kuiambia kamati kuwa hata utaratibu wa mawasiliano baina ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na SUZA haukuwa vizuri, sehemu kubwa ya mawasilizo ilikuwa

ikifanyika kwa simu badala ya barua, alieleza hata barua ya Wizara kwenda kwa SUZA kuijuilisha kuhusu kupewa mradi huo, Makamu Mkuu wa Chuo alidai hakuwahi kuiona barua hiyo, licha ya katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kudai kuwa ilipelekwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilimuhoji Makamu Mkuu wa Chuo Mstaafu Profesa Idris Ahmad Rai ambaye wakati anahojiwa na Kamati maelezo yake yalitafautiana na Wizara ya Elimu kuhusu mtizamo huo na alieleza kwamba tangazo la kazi lilikuwa la wataalamu binafsi (individual consultancy) ambapo watendaji wa Chuo waliomba moja kwa moja bila ya yeye kuwa na taarifa, ingawa walimjulisha baadaye. Hata hivyo, kwa upande wake alitoa barua ya kuwatambulisha washauri elekezi kwa Wizara ya Elimu kwa ajili ya kazi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya uchambuzi wa maelezo hayo ya mashahidi, ni dhahiri kwamba katika utekelezaji wa mradi huo, kumetokea tofauti ya mitazamo baina ya pande mbili, Wizara ya Elimu na SUZA. Wizara ya Elimu imefahamu kuwa mradi huo unatekelezwa na SUZA ambao ndio waliofunga nao Mkataba, ambapo Dkt. Hassan alisaini kwa niaba ya SUZA, lakini kwa upande wa SUZA, kupitia Makamu Mkuu wa Chuo Mstaafu, Profesa Rai, walifahamu kuwa ni Mradi unaotekelezwa na watu binafsi akina Dokta Hassan na wenzake.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kufanya uchambuzi zaidi wa maelezo ya mashahidi Kamati imebaini kuwa huwenda kinachodaiwa kuwa mapungufu ya mkataba, kama alivyoeleza Mwanasheria Mkuu, kuwa ni jambo lililofanywa kwa makusudi baina ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na baadhi ya watendaji wa SUZA waliodaiwa kujimilikisha mradi huo, kwa nia ya kuitenga SUZA na mradi huo, kwa ajili tu ya maslahi yao binafsi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imepata taarifa kuwa yapo mawasiliano yaliyofanyika kwa njia ya simu baina ya kiongozi mmoja mwandamizi wa Wizara ya Elimu wa Wakati huo na Mtendaji Mkuu mwengine wa SUZA wa wakati huo, kumjulisha kuhusu uwepo wa mradi ambao wanakusudia kupeleka SUZA kabla ya hata tangazo la zabuni la mradi huo kutoka.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na mitizamo tofauti iliyotokea baina ya chuo na watekelezaji wa mradi kuhusiana na malipo, ndipo Wizara ilitaka ushauri wa kisheria kutoka kwa Mwanasheria Mkuu kuhusiana na Mkataba wa Mradi huo *(kiambatanisho namba 9)* Mwanasheria Mkuu alijiridhisha kuwa Mkataba uliofungwa baina ya Wizara ya Elimu na Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA) haukupata ushauri wa kisheria. Pamoja na mapungufu hayo, Mwanasheria Mkuu aliagiza mkataba huo uendelee kuheshimiwa na kufuata masharti yaliomo kwa kuweka mbele maslahi ya umma. Pamoja na ushauri huo bado matatizo ya utekelezaji wa mradi yaliendelea.

**Mheshimiwa Spika,** mgogoro wa utekelezaji wa mkataba huo uliendelea baina ya SUZA na waendeshaji mradi ambapo hatua mbalimbali zilichukuliwa na Baraza la chuo ikiwemo kamati za ufatiliaji na kutoa mapendekezo mbali mbali. Aidha, kutokana na migogoro ya matumizi ya fedha za mradi, Serikali nayo ilichukua hatua ya kuagiza uchunguzi maalum kupitia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na kupelekea kutoa repoti maalumu (kielelezo cha repoti ya CAG) yenye mapendekezo yaliopelekea Baraza la Mapinduzi kutoa maelekezo sita kuhusiana na mradi huo (kielelezo namba 10 barua ya tarehe 16 Julai, 2019 yenye kumbukumbu namba IKL/TS/WE-19/VOL.11/62).
miongoni mwa maelekezo hayo ni kama ifuatavyo;

(i) SUZA irejeshewe fedha zake zote ilizopaswa kupata kutokana na Mradi huo kutoka kwa Dokta Hassan Rashid Ali aliyepewa fedha kinyume na utaratibu kulingana na sera na taratibu za chuo kuhusu wataalamu wa chuo wanapopewa kazi kama hiyo kupitia chuo na kutumia rasilimali za chuo.

(ii) Fedha zote zilizotumika kinyume na utaratibu wahusika watakiwe kuzirudisha na kama hawakufanya hivyo wakatwe moja kwa moja kutoka katika mishahara yao.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kadhia hii, na katika kutafuta ukweli zaidi, Kamati ilimuhoji Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wa sasa ili kujua wanavyoifahamu kadhia hii na hatua iliyofikia hadi sasa.

Mheshimiwa waziri alieleza Kamati kwamba jambo hili analifahamu kwa kiasi tangu alipokuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya awamu iliyopita na hivi sasa amelifahamu zaidi baada ya Makamu Mkuu wa Chuo wa hivi sasa Dokta Zakia Abubakar kulileta tena Wizarani na baadaye kuibuka Barazani na kuanza kulifatilia kwa undani zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** Mheshimiwa Waziri alishauri kuwa suala hili ni la kisheria zaidi na linahitaji kuangaliwa kwa umakini hasa kwa upande wa Mkataba kabla ya kulichukulia hatua zaidi.

Kamati ilimuhoji kwanini hakuchukua hatua mapema jambo hili lilipoletwa kwake na hata lilipoibuka Barazani alionekana kama kwenda kinyume na maagizo yaliyotolewa na Baraza la Mapinduzi na yale ya Mwanasheria Mkuu kwa kueleza kuwa bado wanahitaji kulichunguza Zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** Mheshimiwa Waziri aliambia Kamati kuwa Uongozi wa SUZA ulimtaka Katibu Mkuu mpya achukuwe hatua ya kurejeshwa fedha hizo kwa wahusika kukatwa mishahara yao, jambo ambalo Mheshimiwa

Waziri alishauri lisubiri kwanza mpaka wajiridhishe vya kutosha ndipo wachukuwe hatua hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Mheshimiwa Waziri alieleza Kamati kuwa hakupinga maagizo ya Baraza la Mapinduzi bali kulikuwa na maelekezo mengine kutoka kwa Mheshimiwa Rais kuwa Mawaziri wahakikishe hawafanyi maamuzi ambayo yatapelekea Serikali ishitakiwe na kulipishwa fidia, hilo ndilo alilokuwa analichunga lisitokee kwa kuwa alishasikia kuwa wahusika walikusudia kwenda mahakamani endapo wangekatwa mishahara yao.

**Mheshimiwa Spika,** Kuhusu majibu ya Mwanasheria Mkuu ambaye kabla walikuwa pamoja kama Wajumbe wa Baraza la Chuo cha SUZA, Mheshimiwa Waziri alisema hakutia shaka maelezo yake kwa vile alidhani Mwanasheria Mkuu alikuwa na taarifa zaidi yake kwa vile yeye wakati ule aliondoka Baraza la Chuo baada kuteuliwa kuwa Naibu Waziri Wizara ya Elimu na kuliacha suala lile likiendelea.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya uchambuzi wa maelezo hayo ya mashahidi mbali mbali, Kamati inahitimisha hoja hii kwa kueleza kwamba ukweli huu ulioelezwa hapo juu unathibitisha maelezo ya Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir yalikuwa sahihi kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Maadili. Maelezo aliyoyaeleza:

(i) Ni kweli yalikuwa kwenye ripoti zote tatu alizowasilisha Barazani na ambazo ndizo alizotumia kunukuu maelezo yake;

(ii) Ripoti zote alizotumia zimewasilishwa pia kwenye Kamati na Kamati imejiridhisha kuwa maelezo yale yalikuwa sahihi;

(iii) Maagizo ya Baraza la Mapinduzi kutokana na Barua ya Katibu Mkuu Kiongozi yamemtaja kwa jina Dokta Hassan Rashid Ali kama alivyonukuu Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir kutokana barua ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ambaye amepata maagizo hayo kutoka Baraza la Mapinduzi kupitia barua ya Katibu Mkuu Kiongozi;

## 5. MAMBO YALIYOBAINIKA KUTOKANA NA HADIDU ZOTE TATU

Kutokana na uchambuzi huo wa hadidu zote tatu Kamati imeibua mambo yafuatayo:

(i) Kamati imebaini kuwa lipo tatizo kwa wajumbe wa Baraza kufahamu vyema Sheria ya Kinga Fursa na Uwezo ambalo linaweza kuwaletea matatizo katika kutimiza vyema wajibu wao, mfano utaratibu sahihi wa Mjumbe kupata taarifa kwa mujibu wa Sheria.

(ii) Kumebainika kwamba kuna tatizo la uwasilishaji wa taarifa kikamilifu kwa wajumbe kwa vile kadhia ya ZISP imekuwa na muendelezo wa hatua mbali mbali ambazo hazikuelezwa kikamilifu Barazani;

(iii) Kumekosekana uwelewa wa kutosha kwa wananchi kupitia Kanuni ya 148 inayoelezea haki ya mtu kujisafisha anapochafuliwa ili apate kujisafisha bila ya kupata ushauri wa kisheria. Kamati imebaini maelezo aliyowasilisha mlalamikaji kuwa yana baadhi ya dosari kwa kushutumu Baraza kujibebesha kazi ya Mahakama na barua ya malalamiko iliyopelekwa kwa Spika nakala zake kusambazwa kwenye muhimili mwengine nje ya Baraza ambalo ndilo lenye dhamana ya kushughulikia kinga, haki na fursa ya Wajumbe wake (angalia barua ya malalamiko)

(iv) Kamati imebaini baadhi ya majibu ya hoja zinazotolewa na Mawaziri katika Baraza yanagongana, hivyo kupelekea wananchi kushindwa kufahamu ni upi msimamo wa Serikali ulio sahihi. Mfano maelezo ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali akifafanua kuhusu hoja ya Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir na Mwanasheria Mkuu yalivyotofautiana.

(v) Kamati imebaini utaratibu alioutumia Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir kupata taarifa alizoziwasilisha haukufata masharti ya Kifungu cha 9 cha Sheria Namba 4 ya mwaka 2007.

(vi) Maneno aliyotumia Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir hayajakiuka kanuni ya 60 kwa vile aliyasema kwa vielelezo kutoka taasisi husika vilivyodhihirisha maneno aliyosema.

(vii) Kamati imebaini pia maneno aliyoyataja Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir hayajakiuka Kanuni za maadili na Sheria nyengine (Sheria Nam.4 ya mwaka 2015 na Sheria Nam. 4 ya 2007).

(viii) Kamati imebainisha kuwa Dokta Hassan Rashid Ali hakudhalilishwa kwa kuwa maelezo ya Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir hayakumtaja yeye kama ameiba, anadaiwa au amechukua fedha, maelezo yale yanailenga SUZA ambayo Afisa Mas-uul (Makamu Mkuu wa Chuo wa wakati huo) ndiye aliyetoa fedha hizo kinyume na utaratibu kwa kuwa yeye ndiye mwenye dhamana ya kuhakikisha utaratibu wa kutolewa fedha unafuatwa.

(ix) Tatizo lote hilo limesababishwa na kutofuatwa Sheria kikamilifu wakati wa utekelezaji wa Mradi wa ZISP, makosa makubwa yalifanyika wakati wa kusaini Mkataba baina ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na SUZA, hali iliyoleta maneno wakati wa utekelezaji wake.

(x) Afisi ya Mwanasheria Mkuu ilipaswa kushauri kwa kutoa mwelekeo bora zaidi wa kisheria wa namna ya kurekebisha dosari zilizobainika na kuepusha mikwamo ya utekelezaji mkataba iliyojitokeza baadae.

(xi) Pamoja na kutokea kwa makoseo ya kisheria, jambo hili limeharibika zaidi kutokana na migogoro ya ndani ya uongozi wa Chuo cha SUZA na baadhi ya wataalamu wake. Migogoro hii imejenga makundi ya kimaslahi ambayo yamelifanya suala hili kuzidi kuharibika na utatuzi wake kuwa mgumu.

## 6. MAONI YA JUMLA NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na Kamati hii ya Maadili kushughulikia suala hili. Kamati imeona busara kutoa maoni ya jumla kama ifuatavyo:

i. Baraza la Wawakilishi litoe taaluma ya kutosha kwa wajumbe kuhusu namna ya kupata na kutumia taarifa wanazopata kabla ya kuziwasilisha na kuzitumia Barazani.

ii. Baraza litowe taaluma kwa wananchi na jamii kuhusu matumizi sahihi ya haki ya kujitetea na athari zake.

iii. Mawaziri wanapokuwa Barazani wafahamu kuwa wanawajibika kwa pamoja kwa mujibu wa kifungu cha **43 (5)** cha Katiba ya Zanzibar, hivyo wanapotoa kauli zinazopingana, Mtendaji Mkuu anatakiwa asimame kutoa kauli ya mwisho ya msimamo ya Serikali ili kuondosha mkanganyiko kwa wananchi.

iv. Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali isiruhusu hali ya makundi na migogoro katika uongozi wa SUZA, kwa kuwa chuo kinapoteza heshima kwa kuwepo uongozi wa makundi.

v. Kamati inapendekeza Serikali kuunda Kamati ya kuchunguza suala la mgawanyiko wa makundi katika chuo cha SUZA na kulikomesha suala hilo.

vi. Uwepo usimamizi wa karibu wa mikataba kupitia Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kusimamia mikataba yote ya SUZA kuithibitisha na vizuri wawe na uwezo wa kushiriki katika hatua za awali za utayarishaji ili kuepusha dosari za baadae kwenye mikataba.

Kwa upande wa mapendekezo mambo yafuatayo yanapendekezwa:

(i) Ofisi ya Spika imwite Dokta Hassan Rashid Ali iwakutanishe pamoja na Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir kuwapa nasaha na kuwatia nguvu kuendelea kutimiza wajibu wao wa kujenga nchi kwa vile wote hawajakosea. Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir katumia haki yake kujieleza kwa mujibu wa Sheria na Dokta Hassan katumia haki yake kujisafisha. Taarifa ya mkutano huo, Spika ailete Barazani na suala hili liwe limemalizika.

(ii) Suala la ZISP ni kubwa sana lina mambo mengi ambayo hayakuwa sehemu ya hadidu rejea za Kamati kuyafatilia licha ya kuyabainisha kwa madhumuni ya kuweka taarifa kwa usahihi, kamati inapendekeza kuwa Serikali itizame kwa kina jambo hili kupitia vyombo vyake ili haki itendeke kwa pande zote.

(iii) Kamati inaitaka Serikali kuiwasilisha Barazani Ripoti ya Ukaguzi Maalumu ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu Mradi wa ZISP ambayo Baraza kupitia Kamati husika itapendekeza hatua stahiki za kuchukuliwa kwa wahusika.

(iv) Kamati inashauri Serikali ifatilie kwa kina suala hili la Mradi wa ZISP na kuileta ripoti yake Barazani katika mkutano unaofuata ili suala hili lifikie mwisho wake, iwapo itashindikana Kamati hii inapendekeza kuundwa kwa Kamati Teule ya Baraza kwa ajili ya kulishughulikia jambo hili kwa undani kabisa.

## 7. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kuwashukuru kwa namna ya kipekee wajumbe wa Kamati ya Maadili na Kinga za Wajumbe kwa kuwa kitu kimoja katika kufanikisha jambo hili bila kujali tofauti zao. Aidha, nawashukuru pia kwa namna walivyoyachambua madai haya kwa umakini mkubwa huku wakizingatia utaifa na misingi ya haki iliyo bora. Kwa heshima na taadhima naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mheshimiwa Panya Ali Abdalla | Mwenyekiti |
| 2. | Mheshimiwa Shamata Shaame Khamis | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mheshimiwa Hamza Hassan Juma | Mjumbe |
| 4. | Mheshimiwa Profesa Omar Fakih Hamad | Mjumbe |

| | |
|---|---|
| 5. Mheshimiwa Juma Ali Khatib | Mjumbe |
| 6. Mheshimiwa Mtumwa Peya Yussuf | Mjumbe |
| 7. Mheshimiwa Aza Januar Joseph | Mjumbe |
| 8. Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| 9. Ndg. Khadija Salmin Awadh | Katibu |

**Mheshimiwa Spika,** aidha, shukurani za kipekee zimwendee katibu wa Baraza la Wawakilishi, Ndugu Raya Issa Msellem, kwa kutekeleza majukumu yake inavyotakiwa na kuipa nyenzo Kamati yetu wakati wote wa kazi yake, Kaimu Mkuu wa shughuli za Sheria Ndugu Othman Ali Haji katika kuisaidia Kamati katika mambo ya Sheria, Wataalamu wetu wa kitengo cha Tehama cha Baraza wakiongozwa na Ndugu Fuad Rashid Omar, Mratibu wa Kamati Ndugu Khamis Hamad Haji kwa kuratibu vyema kazi za kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika. Na watumishi wengine wote wa Baraza la Wawakilishi ambao kwa namna moja au nyengine walifanyakazi kubwa kuisaidia kamati yetu.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini siyo kwa umuhimu nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi wakati wote umekuwa karibu sana na Kamati hii kutupa miongozo na maelekezo ambayo kwa kiasi kikubwa sana yamefanikisha kazi yetu pamoja na ugumu wake.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho kabisa ni matarajio yangu kuwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wataipokea taarifa hii na kuikubali ndani ya moyo hoja iliyopo mbele yetu inayohusu malalamiko juu ya matamshi yasiyofaa ili kuona kwamba Baraza hili litazidi kuendeshwa kwa nidhamu na uadilifu wa hali ya juu bila kuathiri ufanisi wake.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

……………………………

PANYA ALI ABDALLA
MWENYEKITI
KAMATI YA MAADILI NA KINGA ZA WAJUMBE
17 SEPTEMBA 2021